

# **Ufugaji wa kuku wa Kuroila – Sehemu ya pili**

Kuroila ni ndege wa asili ya Kihindi ambao wana faida kubwa na uwezo wa kutafuta malisho yao wenyewe, ni sugu dhidi ya mabadiliko ya hali ya hewa na mayai yao yana maisha marefu. Mayai na nyama ya kuroila vina manufaa ya kiafya kwa binadamu hasa kwa watoto wachanga, kwani huboresha utendaji wao darasani. Inashauriwa kuwapa kuroila malisho ya ziada ili kuepuka matukio ya magonjwa.

## **Faida za Kuroila**

Kwanza, mayai ya kuroila ya manufaa ya kiafya kwa binadamu kwa vile yana virutubishi kama vile yana protini, vitamini, na madini ambayo husaidia kuunda mifupa na meno thabiti.

Pia mayai ya kuroila yanahitajika sana na walaji kwa vile yana viini vyta njano, na hivyo kusababisha ongezeko la kipato.

Zaidi ya hayo, nyama ya kuroila huhitajika sana kutokana na ladha yake nzuri na chanzo cha protini.

Kuroilia pia huleta mapato ya kilimo, na huboresha lishe hivyo kuwezesha maendeleo ya jamii vijijini.

Mwishowe, nyama ya kuroila ni muhimu kwa binadamu kwani husaidia katika ukinzani dhidi ya magonjwa na maambukizi.